Uhuru Alhamisi Februari 12, 2026 Pg 6

# LATRA yawafungia kazi makondakta wa daladala

**NA REHEMA MAIGALA**

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Habibu Suluo amesema tayari wameshaanza kutekeleza agizo lililotolewa na Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa kuhakikisha wanathibitisha madereva wanaosajili makondakta na kutoa adhabu kali kwa watakaonyanyasa wanafunzi.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Suluo alisema hivi sasa wameanza na Mkoa wa Dar es Salaam, kwa sababu ndio wenye changamoto nyingi za wanafunzi kukataliwa kwenye daladala tofauti na mikoa mingine.

Suluo alisema tangu Waziri Mbarawa atoe agizo lake maofisa wa LATRA wameweka mguu sawa katika Mkoa wa Dar es Salaam, kufanya ukaguzi kwa maeneo mbalimbali kuangalia kama kuna unyanyasaji wanafunzi asubuhi na jioni.

"Tumetia nguvu zetu Mkoa wa Dar es Salaam, kuhakikisha tunaliondoa kabisa hili tatizo la wanafunzi kunyanyaswa kwenye usafiri wakati wanapokwenda shule na wanaporudi nyumbani kwao,"alisema.

Naye, Mkuu wa Mawasiliano na Uhusiano wa Umma wa LATRA,Salum Pazzy alisema agizo hilo wamelianza kwa kutoa elimu kwa madereva, makondakta na wanafunzi.

Pazzy alisema tangu agizo hilo litolewe Februali 4 mwaka huu, tayari wametembelea vituo vikubwa vya basi kikiwemo Mbezi, Gongo la Mboto, Mbagala, Kivukoni, Kariakoo Faya, Makumbusho, Bunju, Tegeta, Buza, Kitunda na maeneo mengine ya Mkoa wa Dar es Salaam.

"Maofisa wa LATRA tayari wapo mitaani, tunatekeleza agizo la Waziri Mbarawa kwa vitendo huku tukitoa elimu,"alisema.

Pazzy alisema licha ya elimu inayotolewa, pia wanawaeleza madereva na makondakta wawachukue wanafunzi watano na zaidi kwa lengo la kuwahi shule kwa muda wa asubuhi na jioni.

Hata hivyo, Pazzy aliwataka wanafunzi wote waifahamu namba ya simu ya LTRA0800 11 00 19 na 0800 11 00 20, ambayo ipo ubavuni mwa daladala zote zilizosajiliwa.

"Pindi mnapopata changamoto pigeni namba hiyo na sisi tutafuatilia daladala hilo huku hatua za kisheria zikifuatwa,"alisema.